**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA UFUNGUZI WA MIKUTANO YA MABARAZA YA MAWAZIRI WA MAJI WA NCHI ZA BONDE LA MTO NILE ) UNAOFANYIKA TAREHE 19 AGOSTI 2022 KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA KILIMANJARO-HYATT JIJINI DAR ES SALAAM

**AGOSTI, 2022**

- **Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso (Mb), Waziri wa Maji, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mwenyeji wa Mikutano hii;**

- **Mheshimiwa Josephine Joseph Lago (Mb), Kaimu Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji, Jamhuri ya Sudan Kusini na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Bonde la Mto Nile;**

- **Mheshimiwa Eve Bazaiba Masudi (Mb), Makamu Waziri Mkuu na Waziri wa Mazingira na Maendeleo Endelevu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile Ukanda wa Maziwa Makuu;**

- **Mheshimiwa Mhandisi Dawalbeit Abdalarahman Mansour (Mb), Waziri wa Umwagiliaji na Rasilimali za Maji, Jamhuri ya Kiarabu ya Sudan na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile Ukanda wa Mashariki;**

- **Mheshimiwa Deo-Guide RUREMA (Mb), Waziri wa Mazingira na Kilimo, Jamhuri ya Burundi.**

- **Mheshimiwa Dkt. Mohamed Abd Elaty (Mb), Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji, Jamhuri ya Kiarabu ya Misri.**

- **Mheshimiwa Dkt. Mhandisi Habtamu Itefa (Mb), Waziri wa Maji na Nishati, Jamhuri ya Shirikisho la Ethiopia.**

- **Mheshimiwa James Macharia EGH (Mb), Kaimu Waziri wa Maji, Usafi wa Mazingira na Umwagiliaji, Jamhuri ya Kenya**

- **Mheshimiwa Dkt. Jeanne D'Arc MUJAWAMARIYA (Mb), Waziri wa Mazingira, Jamhuri ya Rwanda**

- **Mheshimiwa Sam Cheptoris (Mb), Waziri wa Maji na Mazingira, Jamhuri ya Uganda.**

- **Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mliopo;**
- **Mheshimiwa Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;**

- **Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kilimo, Mifugo na Maji;**

- **Waheshimiwa Mabalozi wa Nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile;**

- **Eng. Anthony Sanga, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji;**

- **Eng. Sylvester Matemu, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Bonde la Mto Nile;**

- **Dkt. Hellen Natu, Meneja Kanda wa Jukwaa la Bonde la Mto Nile (Nile Basin Discourse Forum);**

- **Wawakilishi wa Wadau wa Maendeleo, Mashirika na Taasisi za Kimataifa;**

- **Watumishi wa Wizara ya Maji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bonde la Mto Nile mliopo;**

- **Wageni Waalikwa Wote;**

- **Waandishi wa Habari;**

- **Mabibi na Mabwana.**

Kwanza kabisa, ninatambua kuwa, mwezi Juni 2022, Jumuiya ya Bonde la Mto Nile ilipata msiba mkubwa kufuatia kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile na Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji wa Jamhuri ya Sudan Kusini, Mheshimiwa Manawa Peter Gatkuoth. Kwa mara nyingine, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa pole kwa familia yake, Serikali ya Jamhuri ya Sudan Kusini na Jumuiya nzima ya Bonde la Mto Nile.

Kwa heshima, niwaomba wote tusimame kwa dakika moja kumwombea kwa Mwenyezi Mungu. Roho yake ipumzike kwa Amani. Amina.

Kwa niaba ya Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kuwashukuru wote kwa kukubali mwaliko wetu wa kushiriki kwenye mikutano ya pamoja katika ngazi ya Mawaziri: *Nile Equatorial Lakes Council of Ministers (NELCOM), Eastern Nile Council of Ministers (ENCOM) na Nile-Council of Ministers (NileCOM)*. Mtakumbuka kuwa, tarehe 22 Februari 2022 tulikuwa pamoja hapa Dar es Salaam katika maadhimisho ya 16 ya siku ya Bonde la Mto Nile. Hivyo, ninafuraha kwa mara nyingine kuwakaribisha katika Jiji la Dar es Salaam linalojulikana kama kisiwa cha amani kwa kusema **Karibuni Sana.** Vilevile, ninajisikia fahari kupata fursa ya kushiriki kwenye ufunguzi wa mikutano hii muhimu ya Mabaraza ya Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile. Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb), Waziri wa Maji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ahsante sana kwa kunialika.

Nafahamu kwamba mikutano hii inalenga kutoa miongozo ya kisera kwa Sekretarieti na Nchi wanachama katika usimamizi endelevu na uendelezaji wa raslimali majishirikishi ya Bonde la Mto Nile. Nimetaarifiwa kuwa malengo mahsusi ya Mikutano hii ni kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi na Bajeti kwa mwaka 2021/2022; kupitia na kuidhinisha Mpango wa Miaka Mitano (5) wa Bonde la Mto Nile (*5-year Basin-Wide Program*); kupitisha Mpango Mkakati wa Bonde la Mto Nile katika Ukanda wa Maziwa Makuu katika kipindi cha 2022-2027; pamoja na kupitisha

Mpango Kazi na Bajeti ya Bonde la Mto Nile kwa mwaka 2022/2023. Haya ni malengo makubwa, ambayo maamuzi yake yanahusu rasilimali za maji katika nchi zote 10 za Bonde la Mto Nile ambako watu wengi wanategemea maji hayo kwa shughuli za kijamii, kiuchumi na mazingira. Hivyo, mikutano hii ni muhimu sana.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Tukiwa tumekutana hapa kwa ajili ya kujadili maendeleo ya Bonde la Mto Nile, ni vyema tukajikumbusha historia ili kutambua kuwa ulimwengu wa Nile una nafasi kubwa kwenye historia ya mwanadamu. Ni kupitia Mto Nile ustaarabu wa kale uliweza kuenea ulimwenguni. Kutokana na ustaarabu huo, maji yalikuwa ni nyenzo muhimu katika kila nyanja ya maisha, utu na maendeleo. Hali hiyo iliamsha haja ya binadamu kuwa na uhakika wa uendelevu wa upatikanaji wa maji ya kutosha na yenye ubora na kwa muda mwafaka.

Ingawa binadamu tunaishi katika mipaka ya kiutawala; maji yapo na yanatiririka katika mikondo ya asili bila kujali mipaka iliyowekwa na wanadamu. Hali hiyo pia inatulazimisha kuwa na ushirikiano unaotambulika ili kuratibu shughuli za binadamu na kuwa na maendeleo endelevu kama ilivyo kwa Taasisi ya Bonde la Mto Nile. Kupitia Taasisi hii, leo tunajivunia mafanikio tuliyoyapata kutokana na juhudi za pamoja katika kusimamia rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile. Natoa wito kuwa katika majadiliano yenu Waheshimiwa Mawaziri mjadili namna bora ya kusimamia, kutumia na kuendeleza rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Hakuna shaka yeyote kwamba ushirikiano ni njia bora katika kusimamia kwa amani rasilimali zetu za maji. Hivyo, Mikutano ya Mawaziri wa Bonde la Mto Nile inatoa fursa ya kutafakari na kufanya kazi pamoja kwa maana halisi ya ushirikiano wa maji shirikishi. Kwa tafsiri rahisi, matumizi sahihi ya rasilimali za maji yanahitaji utashi katika kutangamana kwenye rasilimali hii. Mikutano hii ni muhimu kutokana na ukweli kwamba inaweka misingi ya ushirikiano na kutoa maelekezo ya kisera siyo kwa Sekretariati pekee bali pia kwa wadau wote. Natambua kwamba hatua na mwenendo wa ushirikiano wa majishirikishi unakuwa mgumu kutokana na kuongezeka kwa wadau na watumiaji wa rasilimali za maji. Hata hivyo, ugumu huo uchukuliwe kuwa ni fursa kwa wadau kuja pamoja ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

Utofauti wa tamaduni, uchumi na hatua za maendeleo kwa Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile unaongeza sababu ya kushirikiana ili kuongeza uwezo na kusaidiana kati yetu. Sababu za kushirikiana ni nyingi kwani umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Kwa mfano, kufikia sasa kuna zaidi ya Mabonde **majishirikishi 276** duniani likiwemo Bonde la Mto Nile. Sehemu ya Mabonde hayo inachukua nusu ya ardhi ya dunia; yanakaliwa na watu zaidi ya **bilioni 3** ambao ni kiasi cha **asilimia 40** ya watu wote duniani; yanajumuisha **nchi 145** na yanaakisi **asilimia 60** ya maji baridi ulimwenguni. Vilevile, kuna kiasi cha miambamaji **shirikishi 600** inayohusisha nchi zaidi ya moja. Takwimu hizi za Umoja wa Mataifa zinasisitiza haja kwa Mataifa kushirikiana katika kusimamia uendelezaji wa rasilimali za majishirikishi kama Mto Nile.

Kwa kuzingatia takwimu hizo, ushirikino na ubia kati ya Mataifa katika usimamizi na uendelezaji wa majishirikishi hauna budi uwe na uhusiano wa moja kwa moja katika maisha ya jamii, biashara na shughuli zote za maendeleo zinazohusiana na rasilimali za maji.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Naipongeza Sekretarieti ya Taasisi ya Bonde la Mto Nile kwa kazi nzuri na jitihada wanazozifanya katika kuendelea kuratibu juhudi za pamoja za Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile. Nchi zote wanachama zinaunganishwa na lengo moja la ***kufikia maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa kuwa na matumizi ya usawa, na yenye faida kutokana na rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile.*** Lengo hili la pamoja linatoa nafasi ya kuwa na mfumo wa ushirikiano wenye faida kwa wote ambao utachochea maendeleo na usimamizi bora wa rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile. Taasisi ya Mto Nile imewezesha kuwa na jukwaa la ushirikiano na kujenga ushirikiano wa kikazi wenye tija kati ya Nchi Wanachama, hivyo kuchangia katika kuwa na amani na usalama.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Katika muktadha wa ubia, ushirikiano na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia rasilimali maji ya Mto Nile na faida zake, sisi Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile tunatamani, tuna ndoto na tuna wajibu. Katika Hotuba yangu wakati nikizindua Maadhimisho ya 16 ya Siku ya Bonde la Mto Nile yaliyofanyika hapa Dar es Salaam mwezi Februari mwaka huu, nilikumbusha kuwa ni miaka 20 sasa tupo katika safari ya kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile kupitia kusainiwa na kuridhiwa

kwa Mkataba wa Ushirikiano wa Bonde la Mto Nile. Katika Hotuba yangu nilitoa rai kwa nchi wanachama kubeba ajenda ya kuwa na chombo madhubuti cha kusimamia rasilimali za Bonde la Mto Nile. Hivyo, matumaini yangu ni kuwa Mikutano hii ya Mawaziri itakuja na mikakati ya kufikia lengo hilo mapema iwezekanavyo. **Tunahitaji Kamisheni hiyo leo, sio kesho.**

Kwa mara nyingine, natoa rai kwa Sekretarieti ya Taasisi ya Bonde la Mto Nile kuratibu jambo hili kwa ubunifu na ushawishi kwani hatua ya kuwa na Kamisheni itaimarisha juhudi zetu za pamoja katika usimamizi endelevu, matumizi ya usawa na uendelezaji wa rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile. Vilevile, itakuwa ni kielelezo kwa ulimwengu na wadau wa Mto Nile juu ya ukakamavu wetu katika kupeleka ushirikiano wetu kwenye hatua ya juu.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Bonde la Mto Nile ni kielelezo bora cha usimamizi na ushirikiano katika eneo la rasilimali za maji duniani. Tafiti nyingi zimefanyika katika Bonde la Mto katika maeneo ya usimamizi wa rasilimali za maji; matumizi ya maji; uendelezaji wa rasilimali za maji; uchumi unaotokana na maji; ushirikiano wa mataifa na watu katika matumizi ya maji; maji na amani; na diplomasia ya maji miongoni mwa maeneo mengine. Hivyo, Bonde la Mto Nile lina utajiri mwingi wa elimu ya maji. Ni katika muktadha huo, ninatoa wito kwa Nchi wanachama kupitia uratibu wa Sekretarieti, kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza agenda za dunia za maji. Miongoni mwa agenda hizo ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa ambapo Lengo

Namba 6 linalohusu maji ni kiungo cha kuyafikia malengo mengine; agenda ya usalama wa chakula na nishati kupitia matumizi sahihi ya rasilimali za maji; agenda ya usimamizi wa athari ya mabadiliko ya tabianchi; agenda ya kuimarisha usimamizi wa maji chini ya ardhi; agenda ya uwekezaji katika sekta ya maji; pamoja na agenda ya maji na maendeleo. Sekretarieti; simamieni masuala hayo na kudumisha hadhi ya Bonde la Mto Nile ulimwenguni kwa kuwa kielelezo cha ushirikiano na amani. Tunapenda kuona Bonde la Mto Nile linaendelea kuwa kielelezo cha masuala bora duniani na Dunia ijifunze kutoka Nile.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kama tunavyofahamu, Nchi wanachama zina wajibu wa kuendesha shughuli za Sekretarieti kupitia michango ya kila mwaka. Natambua jitihada za Nchi zote wanachama katika kutoa michango yao kwa Sekretarieti kwa hali na mali. Pamoja na hilo, ninatoa wito kwa Nchi wanachama kuendelea kulipa michango yetu kwa Taasisi ya Bonde la Mto Nile kwa wakati ili kuiwezesha Sekretarieti kuendesha shughuli za uratibu kwa ufanisi. Vilevile, ninawaalika Wadau wa Maendeleo kuendelea kufadhili shughuli za maendeleo ya miradi katika Bonde la Mto Nile. Tunawaomba muongeze nguvu katika eneo la uwekezaji katika kuendeleza rasilimali za maji kwa kujenga miundombinu.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa kuendelea kutuunga mkono katika juhudi zetu za kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile.

Kupitia juhudi za pamoja kati yetu na washirika wetu wa maendeleo, Taasisi ya Bonde la Mto Nile imeweza na inaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ikiwemo ya kuboresha hali ya maji; kusimika vifaa vya kufuatilia mienendo ya maji, hali ya hewa na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ili kuwawezesha watu wetu kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa tija zenye mafungamano na rasilimali za Bonde la Mto Nile. Kwa muktadha huo pia napenda kuipongeza Sekretarieti ya Taasisi ya Bonde la Mto Nile kwa kuendelea kuratibu ushirikiano na washirika wetu wa maendeleo na kutafuta fedha za kutekeleza programu na miradi hiyo. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Wataalam wa Nchi Wanachama ya Ushauri na Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi inayoongozwa na Wizara ya Maji, Tanzania kwa maandalizi mazuri ya Mikutano hii.

Kwa kuwa Taasisi ya Mto Nile hapa ndipo ilipozaliwa, nachukua fursa hii kwa mara nyingine kwa moyo mkunjufu kuwakaribisha washiriki wote na kuwaomba wafurahie urafiki na ukarimu wa Watanzania. Hii ni fursa nyingine ya kutembelea na kusoma kuhusu uzuri wa Tanzania pamoja na kujifunza lugha adhimu ya Kiswahili.

Baada ya kusema hayo, nawashukuru kwa usikivu wenu na natamka rasmi kuwa Mikutano ya pamoja ya Mawaziri wa Bonde la Mto Nile: *Nile Equatorial Lakes Council of Ministers (NEL-COM)*, *Eastern Nile Council of Ministers (ENCOM)* na *Nile-Council of Ministers (Nile-COM)* imefunguliwa rasmi. Ninawatakia mikutano yenye mafanikio.

**Mungu Ibariki Afrika**
**Mungu zibariki Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile**
**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**